

**HOTUBA YA MHE. CAPT. WILLIAM P. GUMBO, MSTAHIKI MEYA WA  
MANISPAA YA MUSOMA ALIYOITOA WAKATI WA UFUNGUZI  
JENGO LA MWEMBENI COMPLEX TAREHE 02.08.2016**

Mhe, Dr. Charles Mlingwa, Mkuu wa Mkoa wa Mara,  
Mhashamu baba Askofu Michael Msonganzila, Askofu jimbo Katoliki Musoma,  
Mhe. Dr. Vincent A. Naano, Mkuu wa Wilaya ya Musoma,  
Mhe. Vedastus M. Mathayo, Mbunge jimbo la Musoma Mjini,  
Ndugu Fiderica G. Myovella, Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma,  
Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo katika uzinduzi rasmi wa majengo pacha ya mwembeni Complex yanayojumuisha maduka ya biashara na jengo la kituo cha mikutano.

Nawapongeza sana kwa uamuzi wenu wa busara uliowezesha ujenzi wa mradi huu adhimu katika Manispaa yetu ya Musoma. Mungu awabariki sana.

Mafanikio ya mradi huu yanadhihirisha wito mkubwa mlionao katika kuihudumia jamii kiroho na kimwili. Wengi wetu tuliokusanyika katika hafla hii tunaweza tusielewe gharama iliyotumika katika ukamilishaji wa majengo haya lakini itoshe kusema kazi kubwa iliyofanyika hapa wote ni mashahidi kuwa kwa kiwango kikubwa ilihitaji na uadilifu, uchapakazi, na weledi katika kukamilisha mradi huu.

**Mhashamu baba askofu,**

Naomba kwa dhati kuwapongeza wote waliohusika katika ujenzi wa majengo haya pacha kuanzia hatua ya awali ya wazo la ujenzi mpaka ukamilifu wake.

Baada ya pongezi hizo, naomba nieleza kwa uchache faida nyingi zitakazopatikana kwa uwepo wa majengo haya pacha katika Manispaa yetu ya Musoma.

Mosi, ukamilishaji wa mradi huu utatoa fursa katika kupanua wigo wa biashara. Wote tunafahamu moja ya changamoto kubwa inayowakabili wananchi wetu ni upatikanaji wa maeneo ya kufanyia biashara, hivyo ujenzi wa mwembeni Complex utapunguza changamoto hii na kuwasaidia wananchi wanaofanya biashara hasa wajasiriamali wenye biashara ndogo kupata mahali rasmi na salama pa kufanyia biashara.

Pili, Mradi utawasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi na taasisi mbalimbali kupata mahali pa kufanyia mikutano na makongamano mbalimbali ikiwa ni pamoja na sherehe za harusi, mikutano, warsha n.k. Mji wetu bado unachangamoto kubwa ya kumbi za mikutano, kwa ujenzi wa ukumbi huu ni dhahiri kuwa utatoa msaada mkubwa katika matukio mbalimbali ya ndani ya musoma na kitaifa yatakayofanyika katika Manispaa yetu.

**Mhashamu baba askofu,**

Kwetu sisi Manispaa ya Musoma ujenzi wa majengo haya ni mkombozi mkubwa katika kupiga hatua kubwa ya maendeleo, ukiachana na faida za kiuchumi na kijamii nilizozieleza awali ipo faida moja kubwa ambayo kila mwananchi ukimsimamisha na kumuuliza atakueleza na hii ni kupendeza kwa mandhari ya mji wetu.

Waswahili wanao msemu usemao "Mzazi ni Mmoja waleaji ni wengi".Kwa maneno mengine tunaweza kusema ujenzi huu hautalinufaisha tu kanisa hata Manispaa kama taasisi itanufaika sana. Matarajio yetu katika mradi huu ni:-

- Kuongeza mapato kupitia leseni za biashara na tozo mbalimbali za serikali.
- Wafanya biashara wetu watapata mazingira mazuri ya kufanyia kazi
- Ushindani wa kibiashara utaongezeka na hivyo kuufanya mji wetu kuwa kitovu cha biashara katika mkoa wetu wa Mara.Nimejaribu tu kudodosa matarajio machache lakini kimsingi yapo mengi tunayoyatarajia kutokana na ukamilishaji wa mradi huu.

**Mhashamu baba askofu,**

Kabla ya kumaliza napenda tena kutumia fursa hii kukupongeza kwa jitihada zako unazozionesha katika uboreshaji wa mazingira ya kusomea hasa mchango ulioutoa kwa kuchangia madawati 50 kwa shule za msingi yenye thamani ya shilingi Mil. 4.

Ninapenda kukuahidi kuwa tutazienzi jitihada hizi na kwa niaba ya Manispaa ya Musoma napenda kukuahidi ushirikiano katika masuala mbalimbali ya maendeleo ya mji wetu na taifa kwa ujumla.

Mwisho nawatakia kila lakheri katika shughuli zenu zote pamoja na utoaji wa huduma za kiroho kwa watu wetu, ninaamini utulivu tulionao kwa kiasi kikubwa unatokana na jitihada zenu. Mungu Awabariki.

Asanteni Sana.